**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu+255262963313/2963314*
*Nukushi: +255 26 296 3316*
*Barua pepe: ps@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Mji wa Serikali Mtumba,*
*S. L. P 2908,*
***40477 DODOMA***

***Kumb.Na JA.173/176/01A/147*** ***06 Novemba, 2025***

# TANGAZO

## NAFASI YA WASAMBAZA NYARAKA WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA

**(Kanuni ya 6 ya Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka (Tangazo la Serikali Na. 172 la 2023)**

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakaribisha maombi ya Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa **Mikoa ya Iringa, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mtwara, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora.** Waombaji wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo.

**Sifa.**

1. Awe Raia na mkazi wa Tanzania mwenye akili timamu ambaye ametimiza umri wa utu uzima;
2. Awe ni mkurugenzi wa kampuni iliyosajiliwa Tanzania au mshirika wa Taasisi iliyosajiliwa;
3. Awe Msambaza Nyaraka halali wa Mahakama (*Court Process Server*);
4. Awe na leseni ya biashara inayohusiana na kazi za usambazaji nyaraka;
5. Awe na Cheti kuhusu kazi za Usambazaji Nyaraka kilichotolewa na Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto au chuo chochote kinahotambulika na serikali;
6. Awe na elimu ya kidato cha nne au inayolingana nayo na anafahamu vyema lugha ya Kiswahili na Kiingereza;
7. Awe mtu safi, raia mwema asiye na kumbukumbu zozote za makosa ya jinai au utapeli;
8. Awe na Cheti cha Usajili wa Kampuni (*Certificate of Incorporation*); na
9. *Awe na ''Tax clearance'';* na
10. Anayeomba nafasi hiyo ya Wasambaza Nyaraka asiwe: -

    (a) amewahi kubatilishiwa cheti chake cha kuwa Msambaza nyaraka kilibatilishwa chini ya Kanuni hizi au sheria nyingine zozote;

    (b) ni Jaji, Hakimu au Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi au mtu

aliyeajiriwa kwa nafasi yoyote kama mtendaji au afisa wa Baraza;

(c) ni wakili anayefanya shughuli za uwakili;

(d) ni mbunge au diwani;

(e) ni mtumishi wa umma na ambaye majukumu yake yana mgongano wa maslahi na kazi za udalali au usambazaji nyaraka; au

Maombi yawasilishwe kwa kujaza Fomu Na.4 ya **Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka (Tangazo la Serikali Na. 172 la 2023).**

Aidha, maombi yaambatishwe na risiti ya malipo ya ada ya maombi ya kiasi cha Shilingi **30,000**/=. Namba ya malipo (*Control Number*) itatolewa katika Ofisi ya Baraza lililo karibu.

Maombi yote yamfikie Katibu wa Kamati kabla ama ifikapo tarehe 28 Novemba, 2025 kupita anuani kama inavyoonekana hapa chini.

**Katibu,**

Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi,
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
S.L.P. 2908,
**DODOMA.**